



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga anapenda kuwatangazia waombaji wa kazi wote walioomba kazi kwa nafasi ya kazi ya muda ya Karani wa Sensa iliyohusisha Karani wa Sensa, Wasimamizi wa Maudhui na Wasimamizi wa TEHAMA, Kuwa usaili utafanyika tarehe 19 hadi tarehe 20 Julai, 2022 na hatimaye kupangiwa vituo vya kazi watakaofaulu usaili huo.

Wasailiwa watakaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- I. Usaili utafanyika kuanzia tarehe 19 hadi tarehe 20 Julai, 2022 **Ofisi za Kata mlikoombea** kwa nafasi za Karani wa Sensa, na wasimamizi wa Maudhui, wasimamizi wa TEHAMA watafanyia usaili Ofisi ya **Halmashauri ya Wilaya Sumbawanga**.
- II. Kila msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi, vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na Kitambulisho cha Mpiga Kura, Kitambulisho cha Uraia au Hati ya kusafiri.
- III. Wasailiwa wanatakiwa kufika na VYETI VYAO HALISI, mfano cheti cha kuzaliwa, kidato cha IV, kutegemea na sifa za mwombaji.
- IV. Wasailiwa watakaowasilisha 'Testimonials', 'Provisional Results', 'Statement of Result' **HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI.**
- V. Kila msailiwa atajigharimia Chakula, Usafiri na Malazi.
- VI. Kila msailiwa azingatie tarehe, muda na kata aliyoombea kazi hii.
- VII. Kwa waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika kama (TCU, NACTE au NECTA)
- VIII. Waombaji ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya Tangazo husika.
- IX. Matumizi ya simu hayataruhusiwa katika chumba cha Usaili.
- X. Muda wa kufika kwa ajili ya usaili ni saa 2:00 asubuhi.

Imetolewa na

Sebastian Waryuba

**MKUU WA WILAYA YA SUMBAWANGA
MWENYEKITI WA KAMATI YA SENSA WILAYA**

